
# RIPOTI YA UTAFITI WA WATALII WA KIMATAIFA WANAOONDOKA NCHINI, 2024
# MUHTASARI







NATIONAL BUREAU OF STATISTICS
NBS
TANZANIA
STATISTICS FOR DEVELOPMENT

BANK OF TANZANIA

## Utangulizi

Sekta ya utalii nchini Tanzania iliendelea kuimarika kwa mwaka 2024, na kufikia kiwango cha juu zaidi ya kipindi cha kabla ya janga la UVIKO-19. Matokeo chanya haya yalichangiwa na kuendelea kwa kuimarika kwa uchumi wa dunia pamoja na utekelezaji wa jitihada mbalimbali za serikali katika kukuza utalii. Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na utengenezaji na uzinduzi wa filamu ya "Amazing Tanzania" iliyoandaliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Filamu hiyo ilionyesha rasilimali mbalimbali za utalii zilizopo Tanzania, ikiwemo Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Kisiwa cha Zanzibar.

Pamoja na uzinduzi wa filamu ya "Amazing Tanzania", jitihada za uhifadhi zilizotekelezwa zilichangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya sekta hii, jambo lililodhihirika kupitia kutambuliwa kimataifa na kushinda tuzo mbalimbali mwaka 2024, ambazo ni Tuzo ya Mahali Bora Afrika kwa Safari (*Safari Destinantion)*, Tuzo ya Hifadhi Bora ya Taifa (Serengeti), Tuzo ya Vivutio Bora vya Utalii Afrika, Tuzo ya Bodi Bora ya Utalii Afrika (TTB), na Tuzo ya Mahali Bora Afrika kwa Sherehe na Matukio (Zanzibar).

Katika kutekeleza adhima ya ukuaji na uendelevu wa sekta ya utalii, Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT), kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Idara ya Uhamiaji (ISD), na Tume ya Utalii Zanzibar (ZCT), waliendelea na jitihada ya pamoja kwa kufanya Utafiti huu unaohusu Watalii wa Kimataifa wanaoondoka Nchini kwa mwaka 2024. Ushirikiano huu unaakisi dhamira ya kupata takwimu bora na kuweka msingi madhubuti wa kupanga maamuzi, mipango ya uwekezaji na kukuza utalii wa Tanzania kama kivutio bora cha kusafiri.

### Madhumuni

Madhumuni ya utafiti wa huu ni kuwa nyenzo muhimu katika kuelewa muenendo ya sekta ya utalii nchini Tanzania. Ili kufikia dhumuni hili, utafiti huu unalenga kutoa takwimu sahihi kuhusu hali na mwenendo wa watalii pamoja na mapato yatokanayo na utalii. Taarifa hizi ni muhimu kwa mipango ya kimkakati, taarifa za hesabu za serikali, takwimu za urari wa malipo, pamoja na kuainisha jitihada za kuongeza masoko na uwekezaji katika utalii.

### Eneo la Utafiti

Utafiti wa mwaka 2024 ulifanyika katika maeneo manane muhimu ya mipaka inayotumiwa zaidi na watalii wakati wa kuondoka nchini Tanzania: ambayo ni Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, Uwanja wa


Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume - Zanzibar, Horohoro, Namanga, Tunduma, Mutukula, na Manyovu. Maeneo haya ndiyo yanayotumika zaidi na Watalii wa kimataifa kutoka Tanzania bara na Zanzibar. Utafiti ulifanyika wakati wa msimu wa kilele wa utalii, kuanzia tarehe 19 Agosti hadi 1 Septemba 2024, ambapo Watalii 7,593 walihojiwa kati ya Watalii wa kimataifa 15,329.

### Utalii wa Dunia Umeimarika Zaidi

Utalii duniani umeimarika kwa kasi sana mwaka 2024 na kufikia watalii bilioni 1.4, sawa na asilimia 99 ya viwango vya kabla ya janga la UVIKO-19. Ukuaji huu ulitokana na ongezeko la mahitaji ya safari, uboreshaji wa miundombinu ya usafiri wa anga, na sera nafuu za utoaji viza, hasa barani Ulaya na eneo la Asia-Pasifiki (Kielelezo Na 1). Kanda ya Mashariki ya Kati ndiyo iliyoonyesha ongezeko kubwa zaidi, huku Afrika na Ulaya zikivuka viwango vya mwaka 2019. Aidha, mapato yatokanayo na utalii duniani yaliongezeka na kufikia dola za Marekani trilioni 1.6 mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 4 ikilinganishwa na 2019, na asilimia 3 ikilinganishwa na 2023.

**Kielelezo Na 1: Idadi ya Watalii wa Kimataifa Duniani, 2012-2024**

*Milioni*





Chanzo: UNWTO Barometer, Januari 2025

Tanzania ilikuwa na mwenendo sawa na wa dunia, ambapo mwaka 2024 iriekodi idadi kubwa zaidi ya Watalii wa kimataifa. Idadi ya watalii iliongezeka kutoka 1,808,205 mwaka 2023 hadi 2,141,895 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 18.5 kwa mwaka na asilimia 40 zaidi ya viwango vya kabla ya janga (Kielelezo Na 2).

**Kielelezo Na 2: Idadi ya Watalii wa Kimataifa Tanzania, 2015–2024**

*Milioni*





Chanzo: Idara ya Uhamiaji

**Masoko Makuu ya Utalii Tanzania**

Utafiti wa mwaka 2024 unaonesha kuwa masoko ya awali ya watalii bado yaliongoza. Tanzania, Marekani iliendelea kuongoza, ikifuatiwa na Italia na Kenya, wakati kwa upande wa Zanzibar, Italia iliongoza ikifuatiwa na Ujerumani na Ufaransa. Kwa mara ya kwanza, China iliingia kwenye orodha ya masoko 15 bora, hali iliyochangiwa na juhudi maalum za kutangaza utalii kupitia filamu ya ''*Amazing Tanzania*'' iliyozinduliwa nchini China. Kwa ujumla, masoko 15 bora yalichangia zaidi ya asilimia 80 ya watalii kwa Tanzania na asilimia 85 kwa Zanzibar (Kielelezo Na. 3 na 4).


**Kielelezo Na 3: Masoko 15 Bora kwa URT**

*Asilimia*



**Kielelezo Na 4: Masoko 15 Bora kwa Zanzibar**

*Asilimia*





Pia, kulikua na idadi kubwa ya Watalii waliokuwa na umri kati ya miaka 25–44, wakichangia karibu nusu ya watalii wote. Nchini Zanzibar, China na Italia ziliongoza kwa idadi ya Watalii wa umri huu, huku Marekani ikiongoza kwa Watalii wa umri mkubwa. Watalii wa kike walikuwa wengi zaidi ya watalii wa kiume, hasa kwa waliotembelea nchini kwa madhumuni ya mapumziko, kujitolea na kutembelea jamaa.

**Sababu kuu ya utalii imeendelea kuwa ni kwa ajili ya Mapumziko na likizo**

Sababu kuu ya utalii Tanzania kwa mwaka 2024 imeendelea kuwa ni kwa ajili ya mapumziko na likizo, ambayo yalichangia asilimia 74.3 kwa Tanzania na asilimia 91 kwa Zanzibar. Sababu nyingine zilikuwa ni kutembelea jamaa na marafiki, biashara, na kujitolea. Watalii waliokuja kwa ajili ya mapumziko walitumia sana huduma za kifurushi, huku wale waliokuja kwa kutembelea jamaa na biashara wakichagua kupanga safari wao wenyewe (Bila kifurushi). Kwa upande wa kikanda, Kenya ilitoa idadi kubwa ya Watalii waliokuja kwa ajili ya shughuli za kidini, wakati Zambia na Jamhuri ya Kidemocrasia ya Kongo (DRC) waliongoza kwa utalii wa kibiashara.

**Kielelezo Na. 5: Mchanganuo wa Watalii kwa madhumuni ya safari**

*Asilimia*




## Mpango wa safari wa kifurushi umeendelea kuwa kinara kwa watalii

Mpango wa safari kwa kifurushi uliendelea kutumiwa zaidi na Watalii wengi Tanzania na Zanzibar. Tanzania, asilimia 56.3 ya Watalii walitumia mpango wa kifurushi, zaidi ya asilimia 49 kwa mwaka 2023. Watalii kutoka Marekani, China, na Australia walikuwa kwa kutumia safari za kifurushi, huku wale kutoka Zambia, Burundi, na DRC wakipendelea kupanga safari zao wao wenyewe. Zanzibar, idadi ya watalii waliotumia kifurushi iliongezeka kwa asilimia 10.4, ambapo Hispania, China, na Afrika Kusini waliongoza kundi hilo. Aidha, watalii waliokuja kwa likizo na mapumziko, elimu, na tafiti za kisayansi walipendelea kifurushi, wakati watalii waliokuja kwa ajili ya biashara, ununuzi na kutembelea jamaa walipendelea kupanga safari zao wenyewe.

**Kielelezo Na 6: Mwelekeo wa Watalii kwa Mpangilio wa Safari, URT**


**Kielelezo Na 6: Mwenendo wa Mipango ya safari kwa Watalii, URT**

Asilimia




**Kielelezo Na 7: Mwenendo wa Mipango ya safari kwa Watalii, Zanzibar**


Asilimia




## Wastani wa muda wa kutalii nchini ulibaki sawa kwa Tanzania na Kuongezeka Zanzibar

Wastani wa muda wa kutalii Tanzania ulibaki kuwa siku 10 ikiwa ni kwa mwaka wa tano mfululizo. Zanzibar, muda huo uliongezeka hadi siku 7 kutoka siku 6 mwaka 2023. Tanzania, watalii kutoka Ufaransa walikaa muda mrefu zaidi (Siku 15), wakifuatiwa na Wajerumani na Wakanada. Zanzibar, watalii waliokaa muda mrefu walitoka Italia, Hispania, Afrika Kusini, na Uholanzi. Watalii waliokuja kwa mapumziko walikaa muda mrefu zaidi, huku wale waliokuja kwa jamaa au biashara walikaa kwa muda mfupi.

**Kielelezo Na  8: Muda wa Kukaa, URT na Zanzibar, 2019 – 2024**





**Watalii wa mara ya kwanza wameongezeka, wakati waliorudia wanategemea uzoefu**

Mwaka 2024, asilimia 65 ya Watalii waliotembelea Tanzania walikuwa watalii wa mara ya kwanza, ikilinganishwa na asilimia 56.4 mwaka 2023. Mwelekeo kama huo ulishuhudiwa pia Zanzibar. Watalii wa mara ya kwanza walitoka zaidi katika masoko ya mbali kama vile Australia, Italia, Marekani, na Ufaransa, huku watalii waliorudia wakitoka zaidi katika nchi jirani kama Zambia, Kenya, na DRC. Watalii wa mara ya kwanza walipendelea safari za kifurushi, wakati waliowahi kutembelea walipendelea kupanga safari zao kutokana na uzoefu na mazingira.

**Kielelezo Na  9: Watalii wa Mara ya Kwanza na Waliowahi Kutembelea, URT na Zanzibar**

Asilimia




**Tanzania kuendelea kuwa kivutio pendwa na maarufu kwa watalii**

Watalii walipendelea kutalii kwa kuangalia wanyamapori, kufanya mapumziko ya ufukweni, kutembelea jamaa na marafiki, pamoja na shughuli za kibiashara. Maeneo yaliyotembelewa zaidi ni pamoja na Kreta ya Ngorongoro, Serengeti, Tarangire, fukwe za Zanzibar, na Mji Mkongwe (Stone Town), ambayo kwa pamoja yalivutia takribani asilimia 63 ya watalii wote. Watalii waliotumia kifurushi walijihusisha zaidi na safari za kuona

wanyamapori, kupanda milima na uwindaji, wakati wale waliopanga safari binafsi walijihusisha zaidi na biashara, ununuzi, na kutembelea jamaa.



*Mandhari nzuri katika Kreta ya Ngorongoro*



*Nyumbu wakivuka Mto Grumeti, Serengeti*



*Fukwe zenye mchanga mweupe - Zanzibar*



*Tembo wakiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire*

## Kuridhika kwa watalii kulipelekea matumizi na mapato zaidi

Watalii waliendelea kuonesha kiwango kikubwa cha kuridhika na hali ya utalii nchini Tanzania. Ukarimu wa watu ulitajwa kuwa kivutio kikuu, ukifuatiwa na mandhari mazuri, wanyamapori, na vyakula vya asili. Mawakala wa utalii na taarifa kupitia ndugu na jamaa vimeendelea kubaki kama vyanzo vikuu vya taarifa kuhusu Tanzania.

Kwa upande wa matumizi, watalii wengi walitumia fedha taslimu wakiwa Tanzania. Matumizi ya wastani kwa mtalii kwa siku yalikuwa dola za Marekani 243 kwa Tanzania na dola 251 kwa Zanzibar, ambapo watalii waliotumia kifurushi walitumia zaidi kuliko wale wa mipango binafsi. Watalii kutoka China waliongoza kwa matumizi, kwa wastani wa Dola 491.8 kwa mtalii kwa siku, wakifuatiwa na wale kutoka Canada na Marekani. Jumla ya mapato ya utalii yalifikia Dola za Marekani milioni 3,903.1 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 15.7 kutoka mwaka 2023, na hii ilichangiwa zaidi na watalii waliokuja kwa mapumziko na waliotumia kifurushi cha safari.

Ingawa uzoefu wa jumla ulikuwa mzuri, watalii walitaja maeneo kadhaa yanayohitaji kuboreshwa. Maeneo haya ni pamoja na hali ya barabara, taratibu za kupata viza, na jitihada za uhifadhi mazingira. Watalii walibainisha kuboreshwa kwa maeneo haya kutaiwezesha Tanzania kuwa na ushindani zaidi kimataifa. Aidha, pamoja na jitihada za kuboresha huduma za utalii, watalii wanahimizwa kutumia mfumo wa kupata viza kwa njia ya mtandao ambao ni rahisi zaidi, unaokoa muda, na ni rafiki kwa mtumiaji na una uwazi.



WIZARA YA MALIASILI NA UTALI
WWW.MALIASILI.GO.TZ

BENKI KUU YA TANZANIA
WWW.BOT.GO.TZ

TUME YA UTALII YA ZANZIBAR (ZCT)
WWW.ZANZIBARTOURISM.NET

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU (NBS)
WWW.NBS.GO.TZ

IDARA YA UHAMIAJI
WWW.MOHA.GO.TZ